

TAARIFA KWA BUNGE KUHUSU HALI YA AMANI NA USALAMA NCHINI SUDAN

Tarehe 15 April, 2023, nchini Sudan, kulizuka mapigano kati vikosi vya Serikali (*Sudan Armed Forces - SAF*) na Vikosi vya Usaidizi wa Jeshi (*Rapid Support Forces -RSF*), katika Mji Mkuu wa Sudan, Khartoum na katika maeneo mengine nchini humo. Taarifa zilizopo zinaonyesha kuwa mapigano hayo yamesababisha vifo 185, majeruhi zaidi ya 1000, na uharibifu wa mali, ikiwa ni pamoja na ndege. Aidha, mapigano hayo, yamechangia kurudisha nyuma jitihada zinazoendelea za kutafuta amani nchini Sudan.

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inasikitishwa na hali ya kuzorota kwa amani na usalama, na imeendelea kufuatilia hali hiyo. Kama Mjumbe wa Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika, Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaunga mkono Tamko lililotolewa na Baraza la Amani na Usalama la Umoja wa Afrika, katika Mkutano wake uliofanyika tarehe 16 Aprili, 2023, kulaani mapigano yanayoendelea nchini Sudan, na inatoa wito kwa pande zote mbili katika mgogoro huo, kusitisha mapigano yanayoendelea. Tanzania inazitaka pande mbili zinazohasimiana kutatua mgogoro huo kwa njia ya amani,

huku zikihakikisha mahitaji ya kibinadamu, usalama na ustawi wa raia wa Sudan na raia toka nchi nyingine.

Serikali imeendelea kufanya mawasiliano ya mara kwa mara na Ubalozi wetu uliopo Khartoum, ili kujua hali inavyoendelea. Tunao Watanzania takriban 210 nchini Sudan, ambapo 171 kati ya hao ni wanafunzi waliopo nchini humo kwa masomo, na wengine ni maafisa Ubalozi, na raia wengine. Hadi sasa hakuna Mtanzania aliyeripotwa kuathiriwa na mapigano hayo. Serikali inawahakikishia Watanzania kuwa, inachukua hatua stahiki kwa kushirikiana na nchi jirani, Jumuiya za Kikanda, Umoja wa Afrika na Umoja wa Mataifa, ili kuhakikisha kuwa watanzania waliopo nchini humo, na raia wengine wanakuwa salama.

Juhudi hizi zimewezesha mapigano kusitishwa kwa masaa 24 kuanzia jana tarehe 18 Aprili, 2023 saa 10:00 jioni, ili kutoa fursa za mahitaji ya kibinadamu. Aidha kufuatia juhudi hizi, upo mwelekeo wa kusitisha mapigano na kuruhusu njia za kutatua mgogoro huu kwa amani. Serikali inaendelea kufuatilia, na kuandaa mipango ya kuwachua raia wa Tanzania (*Evacuation*), kadri itakavyohitajika.

Serikali, inatoa pole kwa wananchi wa Sudan, na raia wengine na wote walioathirika na kuzorota kwa hali ya

amani nchini humo, kwa namna moja au nyingine, na tunaendelea kuzitaka pande zote mbili zisitishie mapigano na kurudi kwenye meza ya mazungumzo kwa ustawi wa Sudan, Afrika na Dunia kwa ujumla.